



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

OMBI LA KUONYESHA NIA: HUDUMA ZA KUSANIFU NA KUKARABATI OFISI KUMBUKUMBU NAMBA. 0010007463

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inaalika taasisi (kampuni) zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kusanifu na kukarabati ofisi kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, MkoawaTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Kwa minajiri ya Kujenga uwepo wetu jijini Dar Es Salaam, Kampuni ya EACOP itakuwa inawakaribisha wafanyakazi na wazabuni zaidi ya 300 katika mwaka ujao. Ili kupata ofisi katika wiki zijazo, EACOP inatarajia kuchagua mzabuni atakayesaidia kusanifu na kukarabati eneo la ofisi hiyo kulingana na mahitaji ya kampuni yetu inayokua.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

- Kusanifu, kujenga na kupangilia ukarabati ndani ya eneo lililotengwa.
- Kupata vifaa ndani ya muda kadri inavyohitajika.
- Usanifu na ujenzi wa ndani.
- Upangaji wa nafas iza kukaa.
- Uwezo wa kusimamia kazi husika.

VIGezo MUHIMU:

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Rekodi inayoonyesha uzoefu wa kutosha katika kusanifu, kujenga na kukarabati ofisi ndani ya jiji la Dar es Salaam kwa kipindi kisichopungua miaka kumi.
- Iwe na uwezo wa kusanifu na kurekebisha michoro na ramani inavyostahili kulingana na huduma zilizopo kwenye zabuni.
- Ionyeshe uwezo wa kufanya kazi ndani ya ratiba na bajeti ya Mradi.
- Uwezo wa usimamizi wa Afya Usalama na Mazingira uliohibitishwa kwa shughuli za ukarabati wa ofisi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kazi data ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa konesha katika maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani.
- Leseni ya biashara inayodhibitisha kufanya kazi hii.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.100001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11** alasiri saa za Afrika Mashariki (EAT), tarehe **21 Februari 2022**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **0010007463**.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.